







**Impressum**
Kimechapishwa na Pori la Akiba la Selous/Idara ya Wanyamapori na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kiufundi la Ujerumani (GTZ)
Dar Es Salaam 2005
GTZ, S. L. P. 1519
Dar Es Salaam, Tanzania

**Mhariri:** Dr. Rolf D. Baldus
**Tafsiri:** David Kaggi
©Baldus/Siege
Email: scp@africaonline.co.tz
Simu: 22-2866065
www.wildlife-programme.gtz.de/wildlife
**Picha:** Rolf D. Baldus, Vernon Booth, Rod East, Rudi Hahn, Doug Macdonald, Spike Williamson




# Pori la Akiba la Selous

Rolf Baldus na Ludwig Siege
















# Dibaji

Mpaka sasa, kijitabu cha Mwongozo wa usafiri cha Selous kimekuwa kikipatikana kwenye lugha ya Kiingereza pekee. Toleo la kwanza lilichapishwa mwaka 1989 na kufuatiwa na matoleo yaliyofuata baada ya kupitiwa kikamilifu yalichapishwa mwaka 1999 na 2002.
Makala hizi zimekuwa zikilenga soko la kitalii la nje ya nchi hali kadhalika wageni wataalam walioko hapa nchini Tanzania. Nakala zipatazo 15,000 zimekwisha chapishwa hadi kufikia wakati huu, na toleo la kijitabu kipya cha muongozo wa safari liko kwenye maandalizi. Lakini mpaka sasa hakuna mwongozo kwa lugha ya Kiswahili. Kijitabu hiki kinaziba pengo hili na kutosheleza mahitaji ya wageni wanaozungumza Kiswahili ambao hutembelea Selous hasa vijana. Tunadhani kwamba hiki kitakuwa kijitabu cha kwanza cha mwongozo cha usafiri katika lugha ya Kiswahili kwa maeneo yanayohifadhiwa kisheria nchini Tanzania.

Imekuwa ni nia kubwa ya menejimenti ya Pori la Akiba la Selous ikishirikiana na Mpango wa Kuhifadhi Pori la Akiba la Selous (SCP), kuinua hali ya soko la utalii wa ndani kwa wananchi nchini Tanzania. Kwa bahati mbaya , watanzania wengi wanashindwa kusafiri kwenda Selous kwa sababu gharama za usafiri ni za juu mno kiasi cha kufanya watanzania kushindwa kuzimudu ingawaje viingilio wanavyotozwa Watanzania ni vidogo mno kulinganishwa na vile wanavyotozwa watalii toka nchi za nje..

Kwa muda usiopungua miaka kumi hadi leo, uongozi wa Selous umekuwa ukiwakaribisha na kuwapa fursa wananchi na hasa wanafunzi wa shule na taasisi mbalimbali kulitembelea eneo hilo. Majengo na huduma mbalimbali za kukidhi mahitaji ya wageni zimewekwa huko Matambwe ambako ndiyo makao makuu ya Selous.

Serikali ya Ujerumani imekuwa ikisaidia uhifadhi wa Pori la Akiba la Selous, kupitia shirika lake la Ushirikiano wa Maendeleo ya kiufundi (GTZ) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania kupitia mradi wa Mpango wa Uhifadhi wa Selous.
Utoaji wa kijitabu hiki cha mwongozo umewezekana kwa msaada wakifedha kutoka GTZ.
Tunawashukuru R.H.Hall, G.Mnjeja, P.M.Ngoti na H. Ramadhani kwa kupitia kijitabu hiki.
Kijitabu hiki kimetunukiwa kwa askari wa wanyama pori wa pori la Akiba la Selous na askari wa wanyamapori wa vijiji vya Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) nje ya pori la Akiba la Selous.
Rolf D. Baldus (GTZ), Benson Kibonde (Muhifadhi mkuu Pori la Akiba la Selous) na Ludwig Siege (GTZ).







# Kwa nini pori la akiba la Selous ni eneo maalum?

Likiwa na eneo lipatalo kilometa za mraba 48,000 au asilimia tano ya eneo la nchi kavu ya Tanzania, pori la akiba la Selous ni moja ya maeneo makubwa yaliyohifadhiwa hapa ulimwenguni.
Ni pori kubwa kuliko yote hapa Afrika na lenye maji ya kutosha kiasi kwamba uwezekano wa makazi ya binadamu ungekuwepo.
Ukweli huu unalifanya pori hili kutofautiana na maeneo mengine makubwa yaliyohifadhiwa hapa Afrika kama vile Namib-Naukluft lililoko Namibia ambalo sehemu yake kubwa ni jangwa.
Ukubwa wa eneo unastaajabisha, ni kubwa kuliko nchi ya Switzerland au Denmark, hakuna makazi ya watu, na mwingiliano au mguso wa wanadamu ni kidogo sana.
Wageni wanaolitembelea pori hili hujisikia kuwa kwenye nyika asilia mbali na maeneo yaliyozoea mapito ya kitalii. Wanyamapori waliopo hapo ni wakushangaza, makundi ya wanyama (nyati, tembo, viboko, mbwa mwitu na mamba) ni makubwa kuliko yote hapa Africa. Mfumo wa mito na maziwa ni wa kipekee hapa Afrika ya Mashariki.

Hakuna mahali pengine ambapo mtu anaweza akafanya safari za mashua (mitumbwi) kupitia mkusanyiko wa wanyamapori wa kushangaza kama ilivyo ndani ya pori hili. Ndani ya Selous kuna aina 440 za ndege hivyo kufanya eneo hili kuwa sehemu maaalum kwa wapenzi wa kuangalia ndege.
Pori lina maeneo aina kwa aina yakiwemo maeneo wazi yenye nyasi fupi, misitu ya miombo, hali kadhalika misitu kando kando ya mito. Mabwawa ni sehemu muhimu kwa maisha ya mimea ya ardhi oevu, jamii ya mijusi na makazi ya ndege wanaohama hama. Likiwa na eneo kubwa la misitu ya miombo kunalifanya pori la Selous kuwa eneo kubwa la misitu iliyohifadhiwa. Umoja wa Mataifa ulilipa Pori la Selous hadhi ya kuwa eneo la Urithi wa Ulimwengu (World Heritage Site) kwa sababu lina ikolojia ya kipekee.
Pori la Selous ndilo pekee hapa Africa lililobakia katika hali halisi ya asilia. Kutokuwepo kwa shughuli kubwa za Utalii kunachangia kuwepo kwa hali ya nyika. Ili kuhifadhi mazingira hayo na vile vile kuzuia utalii mkubwa, ni utalii mdogo unaodhibitiwa ndio unaoruhusiwa.





# Maelezo ya mfumo wa ikolojia

Sehemu kubwa ya eneo la kanda ya kaskazini ya Selous imetengwa kwa matumizi ya utalii wa picha. Ni moja ya maeneo mazuri na yenye wanyama wengi kupita maeneo mengine ya mfumo mzima wa ikolojia. Kanda hii imepakana na reli ya TAZARA kwa upande wa kaskazini, mashariki ni mpaka wa pori lenyewe na kwa upande wa magharibi ni Stiegler's Gorge pamoja na barabara iendayo Matambwe na kwa upande wa kusini mpaka ni mto Rufiji. Eneo hili ndilo linaloelezewa ndani ya kitabu hiki cha maelezo. Maeneo mengine ya upande wa kusini wa mto Rufiji na Ruaha hayajaendelezwa kwa shughuli za utalii wa picha. Robo tatu ya pori la Selous ni misitu ya miombo iliyojaa miti aina ya mitundu, muwa, mininga na milama. Magharibi mwa pori ni mbuga za nyasi pamoja na miti ya mitagalala, nyasi fupi na tambarare zinazopata mafuriko kwa nyakati za mvua - sehemu hizi hujulikana kama "mbuga" au udongo wa mfinyanzi - sehemu ngumu kwa waendao kwa magari nyakati za mvua. Uoto huu (savannah) huwa ni malisho mazuri kwa wanyama aina nyingi hasa nyumbu. Makundi mbali mbali ya wanyama huonekana kwenye maeneo haya mara kwa mara .

Misitu ya mabondeni na vichaka visivyoingilika vya Pori la Selous huwa maficho mazuri ya wanyama.

Mto mpana wa Rufiji na muelekeo wake wa kuzunguka zunguka hali ambayo inafanya kuwa na maeneo mengi ya ardhi oevu za maziwa na mabwawa na vijito/makorongo, ni moja ya mfumo wa ikolojia wa ajabu katika eneo lote la mashariki mwa Afrika.

Mikoche yenye urefu hadi mita 25 hukua kando kando ya mto Rufiji, aina hii ya mimea huhitaji maji mengi na hufa kama maji yanapungua sana ardhini. Uoto huu wa Rufiji ni makazi ya aina mbali mbali za wanyama kama tembo, viboko, mamba, wanyama wenye kwato na ndege. Miombo ina uwezo wa kuhimili ardhi isiyo na rutuba na mvua chache. Wastani wa mvua ni kati ya millimita 750 kwa upande wa mashariki hadi millimita 1300 upande wa magharibi. Mvua zinanyesha tokea mwishoni mwa Novemba hadi Desemba na kufuatiwa na kipindi cha jua (ukame) miezi ya Januari na Februari na kuendelea tena hadi Mei. Miombo ni misitu iliyorekebishwa kwa karne nyingi na mioto inayotokea kila mwaka au inayoanzishwa na wavuna asali au wawindaji. Nyakati za ukame kuna hali kama vile pori zima la Selous linaungua. Maeneo yanayochomwa mapema huota majani na nyasi changa na wanyama hupata malisho. Maeneo yanayochelewa kuungua huota nyasi nyakati za mvua tu. Mioto hii ya kila mwaka huzuia ukuaji wa miti, lakini miti mingi ya miombo haifi kwa moto. Kuna ubishani tofauti kuhusu mioto hii kwa vile inaonekana kudhuru mimea na viumbe wadogo, hivyo kudhani kwamba ni lazima kujaribu hatua za kuzima mioto hii. Wengine husisitiza kwamba mioto hii ni lazima kutokea na ni sehemu ya mfumo wa ikolojia. Kwa sababu hii mioto huanzishwa na (menejimenti) utawala wenyewe kwa vile inafikiriwa kwamba ni vema kuchoma moto mapema ili usidhuru zaidi uoto kama mioto inayotokea nyakati za ukame ambapo nyasi zote ni kavu na ni wakati wa joto kali.







# Wanyama wenye ngozi nene

Mkazi muhimu wa misitu ya miombo ni mbung'o ambaye ingawaje hana madhara kwa wanya mapori lakini ni muuaji wa ng'ombe. Mbung'o amezuia au kukatisha tamaa makazi ya binadamu na mifugo ndani ya Selous.
Wahifadhi wengine husema mbung'o ni mlinzi bora wa wanyamapori.

Pori la akiba la Selous linajulikana sana kwa kuwa na tembo wengi. Kwa bahati mbaya kutokana na mfululizo wa ujangili wa biashara ya meno, hadi ilipofikia mwanzoni mwa miaka ya tisini (1990), hesabu ya tembo ilipungua kutoka 110,000 ilivyokuwa mwaka wa 1976 na kufikia chini ya tembo 30,000 ilipofikia 1989. Mafanikio ya hatua za ulinzi wa uhifadhi kutokea mwaka 1989 yamewezesha ongezeko la tembo kufika 55,000 ilipofika mwaka wa 1998. Zaidi ya asilimia hamsini ya tembo wote wa Tanzania wapo Selous. Ni wapi pengine tembo wangeweza kuishi kama siyo hapa?
Sio mara nyingi tembo kuonekana wakiwa kwenye makundi makubwa sana ndani ya Selous, bali tembo huonekana wakitembea kwa vikundi vidogo vidogo vinavyoongozwa na kiongozi. Madume ya tembo hupendelea kukaa ndani ya vichaka lakini hujiunga na makundi ya kike mara kwa mara.
Ujangili uliokithiri mnamo miaka ya themanini umesababisha kuwepo kwa tembo wachache wenye meno makubwa, makundi machache ya madume na tofauti kubwa ya mfumo wa marika. Tembo wa rika ya miaka 30 ni wachache. Madume wenye meno ya uzito wa ratili 80 na zaidi wanaongezeka kidogo kidogo na hawapatikani sana. Tembo wanatengeneza mazingira ya mahali wanapoishi. Misitu ya miombo huwa na wanyama wachache lakini wapitapo tembo huvunja matawi na miti na kuwezesha kuwepo kwa nafasi wazi. Uwazi huu huwezesha nyasi na aina nyingi za mimea ambayo hufanya uwezekano wa mchanganyiko wa malisho ya aina mbali mbali za wanyama, hivyo kuleta ongezeko la wanyama aina mbali mbali. Kwa hiyo kile kinachoonekana kwamba ni tabia ya tembo ya uharibifu wa mazingira ndicho kinachojenga hatua na tofauti mbali mbali za uoto wa mimea. Tembo ni mtengenezaji wa uoto wa miombo na maeneo ya uwazi (savannah) ya Selous hivyo basi kama mnyama huyu atatoweka si ajabu uoto utabadilika na aina nyigine ya mimea itaathirika. Ingawaje tembo ni wanyama wa pole ni lazima watu wawe waangalifu na wasi wakaribie karibu.
Kama dume mdogo wa tembo au kiongozi anachezesha masikio yake, anasimamisha mkonga na anasonga mbele, kwa kawaida anajifanya kutishia ila kama kuna adui. Yataka moyo kukutana na tembo anayetishia. Askari wanyamapori wenye uzoefu ndio wanaoweza kutambua kama tembo anatishia tu au amekasirika. Inashauriwa kuwa mwangalifu.
Vifaru weusi ndio walioathiriwa na ujangili zaidi ya aina nyingine zote za wanyamapori wa Selous.







# Wanyama wenye ngozi nene

Jina faru mweusi linapotosha sana kwa sababu siyo mweusi kuliko faru mweupe anavyoitwa mweupe. Faru mweusi ana mdomo wa juu uliopinda kama ndoano unaomuwezesha kula majani ya miti. Faru mweupe ana mdomo wa mraba hula nyasi na hapatikani hapa Tanzania. Faru jike ni mzito kuliko dume, uzito wake unafikia kilo 1,300. Faru weusi hutembea mmoja mmoja siyo kama faru weupe wanaotembea wawili wawili au kwa makundi.

Kinachoonekana kuwa pembe, siyo pembe halisi ila ni nywele nyingi zilizosukana na kugandamana bila kuwa na kiini cha pembe.

Ikitokea kuvunjika inakua tena. Ushauri wa kuwakata faru pembe iwe njia ya kuwa kinga dhidi ya ujangili uliwahi kutolewa. Kilicho sababisha ujangili wa faru ni biashara kubwa ya vipusa.

Huko Asia kuna mahitaji makubwa ya vipusa ambavyo hutumika kwenye dawa za kiasili zinazotumiwa kuponyesha magonjwa mbali mbali ya homa na hata yale ya moyo. Ni mara chache sana vipusa vinatumika kwa dawa za kuongeza nguvu za kiume kama wengi wanavyodhania. Soko kubwa la vipusa liko Yemen ya kaskazini ambako hutumiwa kwa kutengenezea mipini ya majambia kitu ambacho humfanya mtu mwenye jambia la namna hiyo aonekane kuwa tajiri na mwenye uwezo.

Biashara ya aina yo yote inayotokana na mazao ya faru ilifungiwa toka mwaka 1973 kwa mujibu wa mabadiliko ya biashara ya kimataifa ya viumbe na mimea iliyo hatarini kutoweka (CITES). Kufungwa kwa biashara ya vipusa hakukusaidia kuokoa maisha ya faru kwa vile majangili walilipwa fedha nyingi sana kwa vipusa, kitu ambacho kiliwafanya waongeze juhudi zao za kuua faru. Mwanzoni mwa miaka ya themanini idadi ya faru waliokuwemo ndani ya Selous pamoja na maeneo yanayolizunguka pori, ilikadiriwa kuwa faru 3,000. Idadi hii ilikuwa ndiyo kubwa zaidi kuliko idadi ya faru waliokuweko kwenye maeneo mengine hapa Afrika. Faru hawa wasioona mbali na mara nyingi wenye hasira, walikuwa wanaonekana kwa urahisi karibuni kwenye maeneo yote ya Selous. Sasa hivi wamebaki wachache sana na wanajificha kwenye maeneo yenye vichaka vinene. Juhudi za pamoja za utawala wa Selous, GTZ, WWF wakishirikiana na mwekezaji wa hoteli ya kitalii, zimeleta ongezeko la faru ingawaje ni kwa hali ya pole pole.


Sasa hivi kuna uwezekano wa kuona faru kwenye maeneo ya utalii. Faru anapoonekana pahali popote ni lazima taarifa itolewe na ikiwezekana ipigwe picha. Picha zinasaidia kutambua faru mmoja mmoja na kuwezesha utawala wa Selous kuweka hesabu ya ongezeko na idadi ya faru. Faru hutambulika kwa kuangalia tofauti ya umbile la vipusa vyao na mkato wa masikio ambayo kila faru ana namna ya pekee. Njia nyingine ya kuwatambua ni kutumia DNA kwa kupima kinyesi. Kwa kawaida kinyesi kina masalia ya malisho ambayo yana alama za jini (genetic finger prints) ambazo huwezesha kumtambua faru anayehusika na kinyesi hicho. Ujangili wa faru ulikoma mwaka 1990. Faru kidogo walisalia ambao kwa hivi sasa wameanza kujitokeza kwenye maeneo ya wazi nyakati za mchana.



# Wanyama wenye ngozi nene

Faru wadogo na wa makamu wanaonekana, nyakati nyingine vidume vidogo vimeonekana vikitembea kutafuta malisho kwenye maeneo ya mbali kutoka maeneo yao ya makazi. Matokeo yote hayo yanatutia tumaini kwamba faru wataendelea kuishi ndani ya Selous. Mnyama mwigine mwenye uzito mkubwa ni kiboko. Kiboko hupatikana kwa wingi ndani ya mito na maziwa ya Selous. Kwa hivi sasa kuna viboko wapatao 40,000 ndani ya Selous. Idadi hii hufikiriwa kuwa kubwa kuliko uwezo wa makazi yake ndani ya Selous hivyo kupelekea kuweko kwa vifo vingi nyakati za mwisho wa vipindi vya ukame, kwa sababu ya kukosa malisho. Viboko hupendelea kukaa ndani ya maji nyakati za mchana lakini usiku hutoka na kutembea nchi kavu kutafuta chakula. Viboko huonekana wakiwa kwenye vijito vidogo na hata kwenye madimbwi yaliyoko mbali na mito. Viboko wanaweza kuzama ndani ya maji zaidi ya dakika tano. Kundi la viboko huweza kuwa na fujo ndani ya maji, lakini hata wanapoelekea kusogelea mtumbwi, huwa ni vitisho tu. Ikiwa wanataka kushambulia hasa, huzama na kufanya mashambulizi chini ya mtumbwi kwa kuusukuma juu. Madume hushambuliana sana na ni kawaida kuona dume akiwa na makovu na hata madonda mabaya .





# Meno na makucha - Wanyama walao nyama

Pori la akiba la Selous lina idadi kubwa ya simba wapatao 3,000 hadi 4,000. Hawa huwa wapo karibuni kila mahali katika maeneo ya kanda ya kaskazini mwa Selous kwenye eneo la utalii wa picha, hasa kando kando ya maziwa na eneo la Beho Beho. Kutokana na hali ya uoto wa misitu na vichaka vilivyopo, inakuwa siyo rahisi simba hawa kuonekana kama ilivyo kwa simba wa Ngorongoro na Serengeti. Utafiti umeonyesha kwamba kuna makundi 11 yenye simba wakubwa 80 na watoto 20 wanaoishi kando kando ya mto Rufiji.


Ngurumo za simba zinazosikika hata kwa umbali wa kilometa 8 huwa ni jambo la kawaida nyakati za usiku, zinatisha kwa mtu ambaye yuko ndani ya hema anaposikia simba anakaribia. Tofauti na imani iliyopo kwamba simba huogopa moto, ukweli ni kwamba simba hawaogopi moto na inashauriwa kwamba mtu anapopiga kambi porini, asitoke na kutembea tembea nyakati za giza. Hema lililofungwa ni salama sana hata kama kundi la simba litaamua kukaa mbele ya hema.

Wanyama wengine kama vile nyoka na mamba wanahusishwa na imani mbaya, lakini simba huhusishwa na alama ya ukuu - mfalme wa wanyama wote, mkuu wa himaya ya wanyama. Simba wana tabia ya simba na siyo kama watu wanavyowadhania. Kama wakipewa nafasi wataiba windo (mzoga) la mnyama mwingine mla nyama kuliko kuwinda wao wenyewe. Jike ndiye anayefanya uwindaji lakini dume anakuwa wa kwanza kula na halafu anafuata jike. Watoto ndio wanaokuwa wa mwisho kula.

Ikitokea kwamba kuna uhaba wa mawindo, watoto wanaweza kubaki na njaa kwa sababu simba wakubwa wakiwemo mama zao hawawabakishii chochote. Watoto wanaweza kufa kutokana na kutelekezwa na mama zao au kuuawa na madume mageni yanayohodhi mama zao.

Kwa kawaida simba hawana adui zaidi ya wanadamu ingawaje mara chache fisi anaweza akala watoto wa simba. Simba hufanikiwa katika uwindaji wake, huwinda wanyama kutokea swala hadi nyati. Inapotokea kwamba simba amepata mnyama mkubwa, humvuta chini mnyama, hung'ata shingo na kuinyonga. Kundi la simba hujumuisha majike na watoto wao, madume hujiunga nao kwa miezi au miaka kadhaa hadi inapotokea kwamba dume wageni wanawaingilia na kuwafukuza. Ugomvi wa madume ni jambo la kawaida nyakati nyigine vifo hutokea kwa wale wanaoshindwa.

Simba hawapendwi na watu wanaoishi kandokando ya Selous kama vile wanavyopendwa na watalii. Miaka mingine wanavijiji wapatao 40 huuawa na simba kwenye maeneo ya karibu na pori la akiba ukiachilia vifo vinavyotokana na mamba, viboko na tembo. Kwa ujumla nchi nzima ya Tanzania hupata vifo vya watu wapatao 200-300 kila mwaka kutokana na wanyama wakali, huu ni ushahidi mwingine unaodhihirisha kiasi cha nchi inavyojitoa mhanga kwa ajili ya uhifadhi. Kwa bahati nzuri hakuna maafa yaliyowapata watalii waliotembelea Selous hadi sasa, lakini ushauri wa kuwa waangalifu hasa kwa watalii waendao kwa miguu unasisitizwa.






# Meno na makucha - Wanyama walao nyama

Chui hawaonekani mara kwa mara kwa sababu hawa ni wanyama wanaotembea usiku na hudhaniwa kwamba chui ni wachache sana. Hivi sivyo ilivyo ndani ya Selous, ukweli ni kwamba ni wengi kuzidi simba.
Chui hawatembei au kukaa kwa vikundi hivyo ni bahati kuona chui kwa vile hujificha mmoja mmoja. Fasheni ya uvaaji wa makoti ya ngozi za chui imekwisha kwa hiyo chui hawa hawauwawi sana kama ilivyokuwa zamani, kwa sababu hii chui hawapo katika fungu la wanyama waliomo hatarini kutoweka.
Chui wana uwezo wa kuishi kwenye aina zote za mazingira ya Selous lakini wanapendelea kukaa kwenye uoto mnene na vichaka. Wanaweza kuishi karibu sana na makazi ya watu. Mara kwa mara inatokea kwamba wana kamata kuku ndani ya kambi ya Matambwe. Chui ni mwindaji hodari na anaweza kukamata mnyama ye yote wa ukubwa kufikia pongo. Ingawaje chui wanapenda pia kula samaki, wadudu na ndege, nyani/kima ni chakula wanachopenda sana. Mara nyingi chui hupandisha mizoga ya mawindo yao hadi juu kwenye panda za matawi ya miti na baadae kurudi kula. Ukiona mikwaruzo ya kucha kwenye magamba ya mti basi ujue chui wapo maeneo hayo.
Duma nao huonekana kwenye maeneo ya kanda ya kaskazini mwa Selous. Duma ni adimu lakini wamepata kuonekana mara nyingi miaka ya hivi karibuni. Huenda ikawa misitu ya miombo siyo makazi mazuri ya duma na labda wameathirika kutokana na kuwepo kwa ushindani kutoka kwa wanyama wengine walao nyama.
Hii inaweza kuwa sababu mojawapo ya kutokuwepo wingi wa mbweha wa miraba miraba ambao hawaonekani kwa makundi makubwa.
Mbwa mwitu wa Afrika wanatoweka japo ni jamii inayolindwa kwa mujibu wa sheria ya CITES. Inakadiriwa kwamba ni mbwa mwitu wapatao 2,000 hadi 4,000 tu ndio waliosalia. Makazi yao ya asili yanaharibiwa na wakulima na wafugaji.
Kwa hivi sasa wametoweka huko Serengeti pengine ni kwa sababu ya ushindani kutoka kwa fisi wa madoa madoa na simba ambao ni wengi na kwa sababu ya magonjwa yanayoambukizwa na mbwa wanaofugwa na wachungaji wa mifugo.
Kwa upande mwingine mbwa mwitu wa Selous wanaendelea kuishi na kuongezeka. Idadi iliyotokana na mtafiti aliyefanya utafiti kwa muda wa miaka mitano inaonyesha kwamba kuna mbwa mwitu wapatao 1,300 pamoja na watoto. Mbwa mwitu 900 kati ya mbwa 1,300 ni wakubwa. Hata hivyo kuna mbwa mwitu wengine wanaoishi katika maeneo mengi ya mfumo wa uoto huu, kwa mfano kuna mbwa mwitu wapatao 140 ndani ya Hifadhi ya Mikumi na idadi nyingine isiyojulikana kwenye maeneo yanayohifadhiwa na wanavijiji (WMA). Idadi hii ya mbwa mwitu ndiyo iliyo kubwa na ya umuhimu sana hapa barani Afrika na Selous ndipo mahali pekee mgeni anapoweza kupata nafasi ya kuwaona mbwa mwitu. Wanapoonekana huwa hawaogopi watu na hivyo huwa jambo la urahisi kuchunguza undani wa maisha yao kijamii kwa karibu zaidi.
Katika maeneo ya utalii, wingi wa mbwa mwitu ni 1 kwa kila kilometa za mraba 17 (ni pamoja






# Meno na makucha - Wanyama walao nyama

na watoto) au mbwa mkubwa 1 kwa kila kilometa za mraba 25. Hii ni idadi iliyo kubwa kuliko pahali pengine popote hapa Afrika. Sehemu nyingine za Selous ambako uwiano wa wanyama kwa chakula ni wachache na hali ya mazingira hairuhusu kuona mbali, wingi wao ni mbwa 1 kwa kila kilometa za mraba 56. Kwa kawaida mbwa mwitu hukaa kwenye makundi ya mbwa wapatao 20. Kundi kubwa sana lililowahi kuonekana lilikuwa na mbwa mwitu 56.
Mbwa mwitu ni wawindaji hodari na hupata mawindo yao kikamilifu, hali hii ukichanganya na ukweli kwamba hawadhuriwi na wanadamu ndio maana wanaishi vizuri.
Mbwa mwitu walioko Selous wanajilinda vema, hawazembei, pia hawapotezi chakula kingi, ila kiasi cha 2% kinacholiwa na fisi madoa, si kama mbwa mwitu wa hifadhi nyingine.
Mbwa mwitu wa Serengeti hupoteza 86% ya chakula chao kwa fisi.
Mbwa mwitu hutegemea sana macho yao kuona mbali na huwinda nyakati za mchana tu.
Mawindo hutanguliwa na vitendo vya kulambana hadi midadi ipande na ukisikia kubweka basi ujue tayari kazi ya kuwinda iko tayari.
Mbwa mwitu wana uwezo wa kukamata mnyama mkubwa kama vile pundamilia. Mbwa mmoja au wawili wanamzingira mnyama na kumuuma mnyama huyo puani na kushikilia, huku mbwa wengine wanashambulia kwa kupasua tumbo na kutoa matumbo. Mbwa mwitu ni wadogo na hawana uwezo wa kuua mnyama mkubwa kwa kung'ata mara moja, hivyo wanaua kwa kumuuma mnyama mara nyingi sana.

Kwa tabia yao hiyo watu wanaona kwamba ni mauaji ya kikatili, hivyo huwaonea na kuwashambulia kila walipokuwa wanawaona. Hadi miaka ya themanini hata wahifadhi maarufu walikuwa wanawaua mbwa mwitu kila wanapowaona ndani ya hifadhi kwa kuwachukulia kwamba ni waharibifu na adui wa wanyama wengine. Kwa ukweli ni kwamba mbwa mwitu ni wachache sana ukilinganisha na wanyama wengine walao wanyama kama vile simba, chui na fisi hivyo wasingekuwa na madhara makubwa hata kama mawindo yangekuwa machache.
Mawindo hayawi machache kwa kuuawa na wanyama walao nyama, ila huathiriwa na ukosefu wa malisho yao. Huwa ni mbwa jike mmoja tu katika kundi anayezaa na huzaa kiasi cha watoto 12. Kundi zima hushirikiana kulea watoto, mbwa mmoja hubaki kwenye pango na kulinda watoto wakati mbwa wengine huenda kuwinda, wanaporudi kutoka mawindoni hutapika chakula na kuwalisha watoto.
Fisi madoa hutembea usiku tu lakini mtu mwenye macho makini anaweza kuwaona fisi nyakati za mchana wakiwa wamepumzika vichakani au kwenye shimo.
Si kweli kwamba fisi hula mizoga tu au mabaki yaliyoachwa na simba. Fisi ni wawindaji hodari pia na mara nyingi simba hula mabaki ya mawindo ya fisi. Fisi wana mbio kiasi cha kilometa 60 kwa saa na wanaweza kufuatia windo lao kwa mwendo mrefu sana.
Kutokea enzi za mwana falsafa Aristotle iliaminika kwamba fisi huwa mnyama mwenye jinsia mbili yaani kiume na kike. Viungo vyao vya uzazi hufanana ingawaje kwa majike ni vikubwa na






# Wanyama wenya kwato

kwa madume ni vidogo lakini ni vigumu kutofautisha kati yao wanapokuwa mbali. Wanaishi kwenye koo kubwa na majike huwa wengi. Majike hutafuta chakula hadi umbali wa kilometa 100 na wanaweza kurudia watoto wao baada ya siku 2 hadi 3. Fisi anaweza kuonekana akiwa peke yake lakini bado ni sehemu ya ukoo fulani na huwasiliana kwa kuitana.
Wito wao unaoanzia kwa sauti ya chini na kumalizikia kwa sauti kali ya juu ni milio ya kawaida nyakati za usiku hapa Afrika. Wageni wanatishika sana. Fisi ni wengi ndani ya Selous na wingi wao unazidi wingi wa simba kwa eneo.

Pori la akiba la Selous ni makazi ya idadi kubwa ya nyati hapa Afrika. Sensa ya 1998 inaonyesha kwamba kuna kiasi cha nyati zaidi ya 110,000. Kuona kundi kubwa la mamia ya nyati likija kunywa maji kwenye mto Rufiji nyakati za jioni ni jambo lisiloweza kusahaulika. Makundi kama haya huonekana kama vurugu lakini kwa kweli huwa yana mshikamano wa mfumo wa kijamii. Nyati wakubwa na wenye nguvu au majike yenye watoto huwa mbele ya kundi, hivyo kupata malisho mazuri siku zote. Wanyama walioko nyuma ya kundi ni wale walio na hali ya unyonge. Jike anayelea anaweza kuwa kiongozi lakini inampasa arudi nyuma baada ya kumaliza malezi (unyonyeshaji). Kundi kubwa linakuwa kinga nzuri dhidi ya wanyama wengine walao nyama kama vile simba, mbwamwitu, n.k. Vikundi vidogovidogo vinakuwa hatarini kushambuliwa na simba kwa urahisi.

Kwa kawaida madume wakubwa huchangana na kukaa pamoja na majike kwa muda wakati wa kulea kwa vile huwa wanapoteza nguvu nyingi wakati wa kupanda na ugomvi na madume wengine. Wanajitenga na kundi la majike ili kupata afya na nguvu kabla ya kurudi na kujiunga tena na majike hao. Nyati wa jinsia zote wana pembe, ila zinatofautiana kwani pembe za madume huwa pana kuliko za majike. Pembe za majike ni nyembamba na mashina yao siyo makubwa, ni rahisi kutofautisha kati ya madume na majike.
Nyati ni walaji wa nyasi lakini matumbo yao yana uwezo mkubwa wa kusaga malisho kuliko wanyama wengine wasiokula nyama hapa Afrika ya Mashariki, wanao uwezo wa kula hata mimea yenye vitawi na majani madogomadogo (fibrous plants) ambayo wanyama wengine hawana uwezo wa kusaga. Simba ndio maadui wakubwa wa nyati.
Kabla ya karne hii, nyati walikufa kwa wingi kutokana na mlipuko wa kimeta kilichoambukizwa na ng'ombe walioletwa na wataliani huko Eritrea kwa ajili ya kampeni yao ya Ethiopia. Mlipuko wa ugonjwa huo ulitanda bara zima la Afrika kutoka kaskazini hadi kusini na kuua nyati wengi na wanyama wengine wenye kwato.
Nyumbu wa Selous ambao hujulikana pia kama nyumbu wa Nyasa huwa wana rangi ya kijivu-manjano na videvu na mikia myeusi. Jina hilo linatokana na ukweli kwamba hapo zamani walikuwa wanapatikana huko Nyasaland ambayo sasa ni Malawi hadi Msumbiji na kusini mwa Tanzania. Kwa sasa hivi aina hii ya nyumbu wapo kwenye pori la akiba la Selous.

# Wanyama wenye kwato

Wanatofautiana sana na nyumbu wa aina nyingine kwa rangi na ukubwa wa mwili. Wana utepe mweupe puani. Jambo la kushangaza ni kwamba nyumbu wote waliopo kusini mwa mto Rufiji wana alama hii, ambapo nyumbu wa kaskazini mwa mto eneo la utalii wa picha ni wachache tu au asilimia 1 ndio wenye alama hii.
Kongoni wanapendelea kuishi kwenye misitu ya miombo lakini huwa wanaonekana mbugani kando kando mwa barabara iendayo Kinyanguru. Pembe zao zinawatofautisha na Kongoni aina nyingine wa hapa nchini. Pembe hizi zina ncha kali na zina umbo la herufi "S" na ni nene na fupi zikilinganishwa na pembe za Kongoni wengine. Kongoni wa aina hii hupendelea kutembea katika makundi yasiyozidi wanyama 15.
Mnyama mwingine anayeonekana kwa wingi ni swala, ni mzuri wa umbile na ana ukubwa wa kawaida. Huonekana wakiwa kwenye makundi ya madume tu au makundi ya majike yanayolea akiwemo dume mmoja. Ni jambo lisiloaminika kwamba kwenye maeneo ya uhifadhi kijamii yaliyoko kaskazini mwa mto Mgeta, swala wanaonekana wakiwa kwenye makundi ambayo kundi moja la madume linakuwa na zaidi ya swala 1,000 hii hutokea nyakati za kukaribia kuanza kwa majira ya mvua.
Swala ni watembezi nyakati za mchana na ni warukaji wazuri hasa itokeapo kwamba wametishiwa . Swala wana uwezo wa kula nyasi, majani na kutumia aina nyingi za makazi, hata maeneo yenye ukame yanaweza kuwahifadhi na kuwa na malisho ya swala wengi.
Kundi la swala likitishiwa , madume hutoa mlio kabla ya kuruka na kutimua mbio.

Mchanganyiko wa swala, pundamilia na nyumbu ni jambo la kawaida. Uwezo wa hisia za wanyama hawa zinasaidiana na huwa salama wanapokuwa pamoja.
Tandala wakubwa ni wanyama walio wachache sana, hawaonekani kwa wingi kama wanyama wengine ndani ya pori hili. Hawa ni wakubwa kuliko aina nyingine za swala, wana masikio marefu, mabega yaliyojaa na miraba myeupe ipatayo nane hadi kumi mwilini. Tandala huonekana wakiwa kwenye vikundi vikundi vyenye wanyama wachache lakini madume wakubwa hupendelea kutembea mmoja mmoja, hawa wana pembe ndefu zilizojinyonga nyonga. Huwa wanajificha vema kwani wanafanana na mazingira ya pahali wanapojificha, hivyo inahitaji macho makali kumuona Tandala aliyetulia chini ya kivuli cha kichaka akijikinga na jua kali na joto. Unaweza kuwaona kwenye maeneo ya vichaka kati ya Mtemere na Mbuyu hasa sehemu ambapo barabara inapita kando kando ya Ziwa Nzerekela au sehemu ya kwanza ya barabara ielekeayo Kinyanguru.
Pori la Selous ndilo lililobakia kama eneo pekee lenye Mbarapi, kuna kiasi cha mbarapi 4,000 na inasadikiwa kwamba kuna kiasi kingine cha mbarapi wapatao 6,000 au zaidi kwenye maeneo ya kingo yaliyoko kusini na kaskazini magharibi mwa pori hili. Hata hivyo wanyama hawa ni wachache katika maeneo ya utalii unaweza kubahatika kuwaona kati ya Kisaki na Matambwe pia na eneo la barabara ielekeayo Stiegler's Gorge toka Matambwe.
Mbarapi walioko Selous ni wadogo kwa mwili na wenye rangi nyepesi ya weupe kulinganisha na



# Wanyama wenye kwato

mbarapi wa maeneo mengine ya Tanzania na pia pembe zao ni fupi. Idara ya Wanyamapori ikishirikiana na Mpango wa Uhifadhi (SCP) imefanya utafiti na kugundua kwamba Mbarapi hawa ni aina ya Roosevelti iliyokuwa imedhaniwa kwamba imo hatarini kutoweka kwani ilikadiriwa kwamba kulikuwa na Mbarapi aina hiyo 100 tu waliobakia huko kwenye hifadhi ya milima ya Shimba iliyoko nchini Kenya. Mbarapi aina ya Roosevelt ni tofauti na Mbarapi walioko katikati na magharibi mwa Tanzania pamoja na wale waliopo huko Afrika ya Kusini. Pofu nao wanapatikana ndani ya pori hili, hawa ni wanyama wakubwa katika jamii yote ya Swala , Pofu dume anafikia uzito wa kilo 700. Pamoja na uzito wote huo, pofu anaweza kuruka kiasi cha zaidi ya mita mbili kwenda juu hata kama akiwa amesimama na siyo kwenye mbio. Mara nyingi wanatembea kimakundi na kundi moja laweza kuwa na Pofu zaidi ya mia moja.

Madume wana rangi ya kijivu zaidi hasa wanapokomaa/zeeka wanaonekana zaidi kwenye maeneo ya wazi ya Kinyanguru na idadi yao imeongezeka sana hivi karibuni. Madume wa Pofu walioko Selous wanajulikana sana kutokana na kuwa na pembe zilizo kubwa kuliko Pofu wengine walioko hapa Afrika ya mashariki.

Tohe nao wapo kwenye maeneo haya. Hawa ni wadogo kimaumbile kulinganisha na Swala na ni wekundu kwa rangi. Ni madume tu ndio wenye pembe zililizojikunja kwa kuelekea mbele. Wanapendelea makazi yenye magugu karibu na mabwawa au maeneo tepe tepe.

Mgeni mwenye macho yanayoona sana anaweza akaona Pongo. Ni wengi kwa kawaida lakini wao hutembea sana usiku. Mchana hujificha kwenye vichaka/misitu minene kandokando ya mito na maziwa. Rangi yao ni nyekundu kahawia na miraba mstatili, na madoa meupe kwa nyuma mkiani. Wanaposhituliwa wanatoa mlio mkali mithili ya kubweka. Pongo hupendelea kuwa mmoja mmoja isipokuwa majike yakiwa na watoto huwa kwenye vikundi vidogo au wawili wawili. Kama utaona mnyama jamii ya Swala anaruka kwa ghafla toka kichakani na mara hiyo hiyo akatokomea basi ujue kwa hakika anaweza kuwa ni Pongo.

Kuro wanapatikana kwa wingi kando kando ya Mto Rufiji na maeneo ya maziwa. Wana utepe mweupe wa mviringo matakoni, na rangi ya kahawia na ni mkubwa kiasi. Majike hawana pembe na wanafanana na jamii ya "Deer" wekundu wa Ulaya.

Pundamilia nao wanaonekana kila mahali, lakini Twiga wapo kwenye maeneo ya kaskazini ya Selous tu, na Mto Rufiji ndio unaokuwa kama mpaka kwani ndiyo sehemu ya mwisho mtu anapoweza kuona Twiga hapa Afrika ya Mashariki.

Taarifa za Bwana Nicholson aliyekuwa mhifadhi kiongozi zinaeleza kwamba Twiga wameongezeka sana katika miaka ya sabini.

Twiga ni nembo/alama ya Taifa hawawindwi popote hapa Tanzania. Hata hivyo ni wenye aibu na hupenda kukaa mbali na wageni.

Ngiri hutembea na kujificha nyakati za mchana, mara nyingi wanaonekana wakikimbia huku mikia ikiwa imesimama au wakiwa wamepiga





# Wanyamapori wengine

magoti miguu ya mbele wakila minyoo, mizizi au matunda. Watu huwa wanasema ngiri wana sura mbaya, kiasi kwamba wanaweza kuitwa wenye sura nzuri. Macho yao hayaoni mbali ndiyo maana huwa kama mtu anawasogelea huwa wanamfuata karibu lakini wana wepesi wa kunusa harufu na kusikia sauti au mshindo. Wanapenda maji sana ndiyo maana hawakai mbali na sehemu zenye maji. Usiku wanajificha kwenye mashimo ya mchanga. Inachukua uzoefu kidogo kutambua kati ya dume na jike, kwani jike ana chuchu nne na dume ana mbili tu. Madume yaliyo makubwa / wazee yana meno makubwa yanayotumika kama silaha kujihami zidi ya simba, chui na mbwa mwitu. Maeneo ya Kinyanguru yana ngiri wengi kwa eneo kuliko pengine popote hapa Afrika.
Nguruwe kwa upande mwingine wanaonekana kwa shida kwa vile wao hutembea usiku na hupumzika mchana kwenye vichaka karibu na maji. Nguruwe anaweza kuwa na uzito wa kilo 80. Mtu anaweza kubahatika kuona Nguruwe kama atakuwa anatembea karibu na Mto Rufiji saa za alfajiri. Kama walivyo Nguruwe wote, hula chochote wanachopata, mizizi, matunda pori, mayai, wadudu au nyama.

Nyani, Tumbili na Kima wanaonekana kila mahali. Mbega wanaovutia kwa rangi zao nyeusi na nyeupe wanaonekana kwenye misitu iliyoko kando kando ya mito.
Kuna aina nyingine ya Kima ambao hujulikana kama kima wekundu wa Uhehe. Hawa wanapatikana kwenye msitu wa Magombera kusini mwa kambi ya Msolwa ambapo reli ya TAZARA inapita eneo la magharibi la pori la Selous. Inakadiriwa kwamba aina hii ya kima wako kiasi cha 400 ndani ya pori hili.
Mamba nao wapo kwa wingi sana kwenye mito na maziwa ya pori la Selous na maeneo yanayolizunguka pori hili. Mamba wanakula samaki kama chakula chao kikuu lakini hula wanyama wengine pia. Wanakamata wanyama hao wanapokuwa wanasogelea maji. Mamba wanapenda na kujali sana uzazi wao. Mamba akishataga na kufukia mayai jike anachunga eneo hilo hadi atakapototoa, halafu anabeba vitoto akitumia mdomo wake, bila kuwadhuru hadi mtoni ambapo atawachunga kwa muda wa miezi mitatu.
Nyoka wapo kila mahali. Mmoja wa mababa wa Pori la Selous Constantine Ionides alipachikwa jina la utani - "Bwana Nyoka" kwa sababu ya kupenda kwake kukamata nyoka wenye sumu na kuwafuga. Nyoka wengi hawana sumu na wanakimbia watu. Si mara nyingi watu kung`atwa na nyoka.



# Tuangalie historia fupi ya eneo hili

Vyombo vilivyotengenezwa kwa mawe na watu wakati tusioujua vimeonekana. Maeneo haya yalijulikana kwa kuwa mapito makubwa ya misafara ya watumwa na pembe za ndovu toka bara kuelekea pwani. Kijiji cha Kisaki ambacho sasa kiko mpakani mwa pori la Selous kilikuwa ni kiungo cha njia kuu mbili za biashara. Misafara mikubwa yenye watu maelfu ilikuwa ikipita mara kwa mara hasa nyakati za kiangazi. Wavumbuzi kama Burton na Speke (1857) na Johnson na Thomson (1879) walipita maeneo haya na Johnson alifia Beho Beho na alizikwa hapo. Wasafiri hawa waliona vijiji vichache, walitoa taarifa kwamba wanyama walikuwa wachache nyakati hizo.


Mwaka 1905 Wilhelm Kuhnert aliyezaliwa (1865 - 1926) aliyekuwa mmoja wa wazungu wa kwanza wanasanaa kuangalia na kuchora wanyama pori wa Afrika maporini, alivuka mto Mgeta na kuingia eneo ambalo sasa ndilo pori la Selous. Alisifia sana eneo la Beho Beho kwa uzuri wake (mandhari yake mazuri) pamoja na ziwa Tagalala.

Miaka mitatu baada ya kuja kwa bwana Kuhnert, Mjerumani mwingine aitwaye Hans Schomburgk alifanya uwindaji katika maeneo ya kaskazini ya Selous na vitabu vyake vingi vinaonyesha picha za wanyamapori kandokando ya mto Rufiji.

Mwaka 1905 vita vya Maji Maji kuupinga ukoloni wa kijerumani vilipamba moto na kupiganwa katika eneo la kusini mwa nchi. Eneo ambalo maji hayo yaliyoaminika kuwa na nguvu za kiganga yalipatikana toka eneo moja karibu na Mto Rufiji na sehemu nyingine yalipotoka ni kwenye kijiji cha Ngarambe kinachopakana na pori la Selous kwa upande wa Mashariki. Mapigano mengine yalirudi Selous wakati wa vita kuu ya pili ya Dunia. Manowari/meli ya kivita iitwayo "Konigsberg" ilipata maficho ndani ya mdomo wa mto Rufiji umbali wa kilometa 100 mashariki mwa Mtemere. Ilipozamishwa na wanamaji wa kiingereza, askari wa kijerumani walifanikiwa kuondoa mizinga 10 yenye vipenyo vya inchi 4.1, wakaipakia juu ya magurudumu na kusafiri nayo maeneo yote ya Afrika ya Mashariki wakati wa kampeni zao za kivita. Mwaka 1917 askari wa wajerumani wakiongozwa na General von Lettow Vorbeck walipigana na askari wa kiingereza karibu na eneo la Beho Beho mahali amba po mvumbuzi/mpelelezi maarufu wa kiingereza Frederick Courteney Selous alifikwa na maafa wakati wa mapigano. Rafiki yake J. G. Millais, alitoa maelezo ya tukio hilo kama ifuatavyo:

Majeshi yetu yalisonga mbele kutoka Kisaki alfajiri ya tarehe 4.1.1917 kwa lengo la kushambulia na kuzingira kiasi kikubwa cha askari wa wajerumani waliokuwa wamepiga kambi chini ya vilima mashariki mwa Beho Beho (Milima ya sukari) kaskazini mashariki mwa barabara inayoelekea Kisaki kusini mashariki mwa Mto Rufiji umbali ulikuwa kiasi cha maili 13 kati yetu na maadui. Vilima vifupi ambavyo ndipo askari wa wajerumani walipojificha, vilikuwa na vichaka vinene vyenye miiba hivyo ilikuwa ni vigumu kuona upande uelekeao magharibi. Hata hivyo walitambua mara moja hatari iliyo karibu nao kwani waliona mzunguko wa




# Tuangalie historia fupi ya eneo hili

sehemu ya kikosi cha 25 cha wapiganaji wa kifalme ambacho kimeagizwa kuwazuia askari wa wajerumani katika barabara ielekeayo kusini mashariki, barabara pekee iliyokuwepo ambayo wangeitumia kurudi nyuma. Inaonyesha wazi kwamba askari wa wajerumani waliamua kurudi nyuma mapema kwa sababu kikosi cha askari wa Waingereza wakiongozwa na Captain Selous walifika sehemu hiyo wakati huo huo kama wao. Mapigano makali yalizuka kati ya pande hizo mbili na Selous aliamrisha askari wake kuwashambulia Wajerumani ambao walikuwa ni wengi na waliwazidi Waingereza na kuwafukuzia vichakani. Ilikuwa ni wakati huu ambapo aliuliwa kwa risasi iliyompiga kichwani.

Frederick Courteney Selous (anayetamkwa Seloo na "s" ya mwisho iliyofichika) alizaliwa 1851 akiwa mtoto wa kiume wa mwenyekiti wa London Stock Exchange. Alipenda sana kufuata nyayo za jasiri wa tangu utoto wake Dr. David Livingstone kuja Afrika, kitu ambacho alifanikiwa mwaka 1871. Aliwinda na kupeleleza nchi ya Matabele huku akiwa mtangulizi kumwezesha Cecil Rhodes kufungua Zimbabwe kwa ajili ya walowezi wa kizungu. Muwindaji hodari na ni muhifadhi wa kwanza, aliandika vitabu vingi vinavyohusu safari zake na historia asilia, vitabu vyake vingi vilikuwa miongoni mwa vile vilivyouzwa kwa wingi sana enzi za utawala wa Malkia Victoria wa Uingereza. Shujaa huyu alipojiunga tena na jeshi alikuwa na umri wa miaka 64 wakati wa vita kuu ya pili ya dunia ilipoanza. Alijiunga na kikosi cha 25 cha wapiganaji wa miguu wa kifalme huko Nairobi na akasaidia kuyafukuza majeshi ya wajerumani yaliyokuwa yakiongozwa na General von Lettow Vorbeck kuelekea kusini mwa Tanzania. Inasemekana kwamba Selous hakutumia usafiri wa aina ye yote bali alitembea kwa miguu pamoja na askari wake wakihimili shida na taabu za mazingira magumu ya hali ya hewa na magonjwa. Hata ilipofika mwishoni mwa mwaka 1916 walifanikiwa kuwafukuzia mbali askari wa wajerumani kutoka kwenye ngome yao kuu ya Kisaki na wakati huo alibakiwa na askari 60 tu kutoka askari 1166 aliokuwa nao awali. Nyakati za jioni wakati askari wake wakiwa wamechoka na kupumzika kwenye mahandaki, yeye alikuwa akikamata vipepeo na kuwinda. Hadi leo familia yake iliyoko Uingereza inatunza nyara ambayo ni fuvu/pembe za mnyama Kudu aliyemuua huko Kisaki.

Mwaka 1896 Gavana wa Kijerumani alifunga uwindaji eneo kati ya mto Mgeta na Rufiji na kulitangaza kuwa Pori la Akiba. Sehemu ambayo kwa sasa imekuwa kivutio kikubwa kwa utalii wa picha eneo la kanda ya kaskazini ya pori la Selous na imekuwa ndiyo ya kwanza hapa Afrika kutangazwa kuwa pori la akiba miaka miwili kabla ya Hifadhi ya Krueger ya Afrika ya Kusini. Baadaye eneo kati ya Ruaha-Kilombero na mto Ulanga upande wa magharibi pamoja na maeneo mengine mawili upande wa mashariki karibu na Liwale yalitangazwa na wajerumani kuwa mapori ya Akiba. Sheria ya kuhifadhi ilitungwa na kuanza kutumika. Nyaraka zilizopatikana hivi karibuni zinaonyesha kwamba mpiga picha na muandishi aitwaye Carl Georg Schillings (1865-1921) aliandika sera ya



# Tuangalie historia fupi ya eneo hili

wanyamapori ikijumuisha kuhifadhi na matumizi endelevu ya wanyamapori jambo ambalo ndilo linalojumuishwa kwenye sera ya wakati huu.
Hadi hi vi leo pori la akiba la Selous hujulikana kwa jina la shamba la bibi na inasemekana chanzo kilitokana na mtawala wa ujerumani Kaiser Wilhelm II, ambaye alimzawadia mke wake pori hilo kama zawadi ya kumbu kumbu ya kuzaliwa ingawa hatukupata ushuhuda wa maandishi kuhusu swala hili.
Baada ya vita Tanganyika ikawa chini ya uangalizi wa Waingereza na pori la akiba likapanuliwa na kupewa jina la Selous hapo mwaka 1922 kwa kumkumbuka mvumbizi/mpelezi shujaa aliyefia humo mwaka 1917.
Mnamo miaka ya 1930 na 1940, utawala wa Tanganyika ulihamisha wananchi waliokuwa wanaishi kwenye maeneo yenye mbung'o ili kuwaepusha na ugonjwa wa malale. Njia iliyotumika kuwazuia watu wasiyarudie makazi yao ya zamani ilikuwa ni kuyatangaza kwamba ni sehemu ya pori la akiba na kuongeza eneo lililokwisha hifadhiwa tangu awali.
Zaidi ya Tembo elfu tatu waliuawa kila mwaka nje ya maeneo yaliyotengwa/hifadhiwa ili kuzuia uharibifu wa mazao. Sera ya wakati huo ilikuwa ni kulinda wanyama walio ndani ya maeneo yaliyotengwa na kuua wanyama wote waharibifu wa mazao na maisha ya watu.
Constatine Ionides muingereza mwindaji maarufu aliyekuwa kwenye kituo cha Liwale pamoja na askari wachache ndio waliokuwa na jukumu la kuwadhibiti wanyamapori ndani ya eneo la maelfu ya kilometa za mraba ikiwa ni pamoja na sehemu kubwa ya pori la Selous.
Asingefanikisha kazi hii nzito bila usaidizi wa maofisa wa kitanzania miongoni mwao akiwa Mzee Madogo ambaye tulimwajiri baadaye akiwa na umri wa zaidi ya miaka sitini ili awafundishe askari na bahati mbaya Mzee Madogo akafariki dunia akiwa ndani ya "shamba la bibi" alilolipenda sana. Brian Nicholson, muhifadhi wa kizungu wa mwisho alitenda kazi nzuri kuibadili Selous kuwa namba moja ya mapori yote ya akiba. Nicholson alianzisha uwindaji wa kitalii ndani ya Selous ambalo lilikuwa halitumiki kwa kuwa alihitaji fedha za kujengea vituo, barabara pamoja na shughuli za kuzuia ujangili ndani ya eneo kubwa la pori. Eneo la mwisho kuunganishwa na pori la Selous ni lile lililopo kusini mwa kingo za mto Rufiji wakati wa kampeni za vijiji vya ujamaa mwaka 1974. Hadi wakati huo kulikuwepo na usafiri wa basi hadi kingo za kusini ya mto mkabala na Kibambawe.

Wakazi wa maeneo hayo walipatiwa makazi mengine kando kando ya barabara ya Mloka - Mkongo. Wananchi hawa waliondolewa kutoka kwenye ardhi nzuri yenye rutuba na maji yenye uvuvi mzuri kwa hiyo ujangili umekuwa ni kikwazo kikubwa na kazi ngumu kwa utawala wa pori tangu wakati huo.



# Janga latokea

Serikali ilipofunga uwindaji wa kitalii mwaka 1975, mapato kutokana na uwindaji yakawa sifuri, wataalamu wa uwindaji wakaondoka porini na kuliacha pori wazi kwa majangili. Uharibifu ukaanza na hadhi ya pori ikaporomoka ikazidi kuongezeka kutokana na uchumi duni wa nchi. Juhudi za kuchimba bwawa kubwa kwa ajili ya umeme zilileta wafanyakazi wapatao 2,000 huko Stiegler's Gorge.

Faru wengi waliokuwepo kwenye maeneo hayo waliuawa. Mwanzoni mwa miaka ya themanini, shughuli za utafiti wa kutafuta mafuta ulifanyika, hivyo barabara/njia nyingi zlizonyooka zilitengenezwa ndani ya pori, na kufungua vichaka na misitu minene. Njia hizi zimevutia majangili kwani zimewawezesha kuingia na kupitia maeneo mengi, makundi makubwa ya majangili mara nyingi yenye watu kiasi cha sitini kwa kundi yamekuwa ya kiingia kufanya uhalifu.

Mwaka 1982 wakati pori la Selous linapewa hadhi ya kuwa urithi wa ulimwengu, mauaji makubwa ya Tembo yalikwishaanza na kupunguza Tembo kutoka 110,000 waliokuwepo mwaka 1976 hadi kufikia Tembo wachache chini ya 30,000 hapo mwaka 1991.

Inakadiriwa kwamba Tembo 20 walikuwa wanauawa kwa mtutu wa bunduki kila siku. Katikati ya miaka ya themanini, vijana wenye dhamira nzuri walipewa uongozi wa Selous. Pamoja na misaada ya mashirika ya uhifadhi kama Frankfurt Zoological Society, Mfuko wa Uhifadhi Duniani hali kadhalika Shirika la Misaada ya Maendeleo ya Kifundi la Ujerumani (GTZ) pamoja na sera nzuri za Serikali, Idara ya Wanyamapori imeweza kubadili hali ya Selous. Kwa sasa pori la Selous ni moja ya mapori yanayotambulikana kimataifa kama moja linaloendeshwa kiustadi na kuhifadhiwa vema hapa Afrika. Idadi ya wanyamapori wakiwepo Tembo inaongezeka na ujangili ndani ya pori ni kidogo sana.

Hakuna mahali po pote duniani ambapo maeneo yaliyotengwa na kuhifadhiwa yanaepuka vitisho vya nje. Sasa hivi kuna mawazo ya kufanya uchimbaji wa madini ya Uranium ndani ya Selous. Cha kutisha zaidi ni mipango iliyokuwepo ya kuchimba bwawa kwenye Mto Ruvu karibu na mpaka wa kaskazini. Bwawa hili lingeleta mafuriko kwenye eneo la sehemu ya kanda ya kaskazini ya Selous lakini cha muhimu zaidi ni maeneo nyeti ya malisho nyakati za ukame nje ya maeneo yaliyohifadhiwa ambayo yangeharibiwa.




# Mpango wa kuhifadhi pori la Selous

Kutokea mwaka wa 1987 pori la Selous limepata msaada mkubwa chini ya makubaliano ya Serikali ya Ujerumani - Tanzania mpango wa kuhifadhi Selous (SCP) kupitia Shirika la Misaada ya Maendeleo ya kuhifadhi la Ujerumani (GTZ). Vikosi vya askari vimepatiwa nyenzo na vitendea kazi, mawasiliano yameimarishwa na mpango wa menejimenti umetengenezwa na ndio unaoongoza shughuli za pori.

Sehemu kubwa ya mpango huu ni ile ya ubakishaji wa sehemu ya mapato (fedha) ambapo Selous inaruhusiwa kubakisha nusu ya fedha zote zilizozalishwa humo. Mapato kwa mwaka ni kiasi cha dola za kimarekani zaidi ya millioni tatu.

Sehemu ya pili ya mpango huo ni ile inayoshughulika na ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa maliasili.

Kati ya matatizo mengi ni pamoja na tatizo la uharibifu wa mazao na upotevu wa maisha ya watu kutokana na wanyama. Pamoja na sheria za kudhibiti uwindaji mahitaji ya nyama vijijini na biashara nzuri mijini na Dar es Salaam yanasababisha uwindaji haramu usiodhibitiwa kwa ajili ya biashara na yote hayo yalizidi kuleta mfarakano kati ya wanavijiji na utawala wa Selous.

Ni filosofia ya SCP kwamba ni vigumu kudumisha uhifadhi kwenye maeneo yaliyotengwa kama hakuna kuwapatia faida wananchi wanaoishi kando kando mwa maeneo hayo. Ili kufanikisha, uhifadhi ni lazima ufanyike - pamoja kwa kupitia kwa watu na siyo kinyume chake.

Vijiji vya kwanza vilijiunga na mpango huu hapo mwaka 1989 na hadi sasa kuna vijiji 57 vinavyoendesha uhifadhi kwa jamii. Wanavijiji wanatenga sehemu ya eneo la ardhi yao kwa shughuli za uhifadhi - kilimo kinazuiwa na uhifadhi wa Mali Asili unaruhusiwa. Hivyo wana vijiji wanaruhusiwa kuwinda kwa mgao maalum kwa ajili ya matumizi yao. Wanachagua askari wao kwa kazi ya doria. Mfumo huu umejumuishwa kwenye sera mpya ya Idara ya Wanyamapori Tanzania na itatumika nchi nzima. Wanavijiji wataweza kujipatia fedha kutokana na biashara ya utalii wa picha na uwindaji kwenye maeneo ya ardhi yao.

Kuna ukweli kwamba ujangili umepungua sana kwenye maeneo ya kinga na hata yale ambayo yana wanyama wengi na kwamba wanyama wanaongezeka na wanarudi hata kwenye yale maeneo ambamo walitoweka kwa miaka mingi.

Idara ya wanyamapori ndani ya Wizara ya Mali Asili na Utalii ndiyo inayotawala na kusimamia Pori la Akiba la Selous. Ofisi/Kituo kikuu cha pori hili kiko Matambwe kanda ya kaskazini. Jumla ya watumishi 350 wakiwemo askari, mafundi na utawala (sawa na kila askari mmoja kulinda kilometa za mraba 140) wanafanya kazi ndani ya Selous.

Kazi zao kubwa ni kufanya doria, kuzuia ujangili na pia wanafuatilia idadi ya wanyama, na kufungua barabara, kuzitunza pamoja na njia zote za mawasiliano, viwanja vya ndege, nyumba za watumishi n.k. shughuli zote hizo zinalipiwa na fedha iliyobaki kutokana na asilimia hamsini ya mapato ya Selous.



# Mpango wa kuhifadhi pori la Selous

Mapato ya Selous yanatokana na vyanzo viwili (I) Mapato kidogo kutoka utalii wa picha (II) Asilimia 80 kutoka uwindaji wa kitalii. Kiasi cha wawindaji wageni wapatao 400 hutembelea pori hili kila mwaka kati ya Julai na Desemba kiasi cha wanyama 3,000 wanauawa kila mwaka. Uwindaji huu ni endelevu kwani mgao wa wanyama wa kuwindwa unatolewa kufuatana na matokeo ya ufuatialiaji wa ikolojia na ni sehemu ndogo tu ya idadi ya wanyama inayotolewa. Wale wasiopenda uwindaji waelewe kwamba bila pato la fedha kutoka uwindaji, kazi ya kuwalinda wanyama na kutunza pori isingewezekana na mapori yangetoweka.
Mpango wa menejimenti ya Selous unaweka bayana sera na vizuizi/vizingiti kwa pori la Selous.
Nia ni kuhakikisha kwamba shughuli za wanadamu zinakua za kiasi kidogo sana. Hii ni pamoja na utalii. Kwa sasa pori lina watalii zaidi ya 6,000 kwa mwaka. Watalii ni lazima wapate na wafurahie hali ya kipekee na mazingira ambayo hayajaharibiwa.
Utalii wa picha unapanuka pole pole ili ifikapo mwaka 2001 kuwepo kambi/hoteli sita zinazohudumia kwenye kanda ya kaskazini ya Selous. Kuna mpango wa kufungua kambi mpya kusini mwa Mto Rufiji.
Mpango wa utalii umetengenezwa kwa kuangalia wakati wa usoni/mbele uwezekano kwamba utalii unaweza kuwa wa vurugu na mkubwa kando kando ya maziwa .

Mradi wa mpango wa kuhifadhi Pori la Selous (SCP) umefikia mwisho wake hapo mwishoni mwa mwaka 2003. Shughuli zote zinazo husu vijiji zinaendelea chini ya mradi wa ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi uliokita (CBC) unaoendeshwa na GTZ kwa ushirikiano na Idara ya Wanyamapori.







